## MKATABA WA KUFANYA BIASHARA ENEO LA JESHI

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe ..1...ya mwezi ...JULAI.....Mwaka 2025.

**KATI YA**

**671 REGT S L P 3142 Dar es salaam** ambaye ndani ya Mkataba huu atajulikana kama **MPANGISHAJI/MMILIKI** (jina ambalo litamaanisha yeye mwenyewe, wawakilishi wake, mtu yeyote atakaye simamia kwa namna yeyote ile) kwa upande mmoja.

**NA**

IMPERIAL ROAD HAULAGE LIMITED........ wa **S L P** ..2150.........**, Dar es salaam** ambaye kwenye Mkataba huu atajulikana kama (jina ambalo litamaanisha yeye mwenyewe, wawakilishi wake, na ikibidi warithi wake) **MPANGAJI** kwa upande wa pili.

**UTANGULIZI**

A **Kwa Kuwa MPANGISHAJI** ni Msimamizi wa Eneo la biashara lililopo ..KITUNDA JESHINI........ ambalo kwa hiari yake mwenyewe amekubali kumpangisha MPANGAJI.

B. Na kwa Kuwa MPANGAJI ni IMPERIAL ROAD HAULAGE LIMITED(Mmiliki/kampuni) binafsi iliyosajiliwa na BRELA na Mamlaka husika kisheria kufanya biashara ndani ya Nchi ya Tanzania.

C. MPANGAJI kwa hiari yake mwenyewe amekubali kupanga Eneo la biashara lenye ukubwa wa Square mita za Mraba..33781... lililopo..KITUNDA JESHINI.. kutoka kwa MPANGISHAJI kwa dhumuni la kufanya biashara ya MAEGESHO YA MAGARI MAKUBWA NA KIWANDA CHA UTENGENEZAJI TRELE NA TRELE ZA SEMI PAMOJA NA GHALA.

**HIVYO BASI,** pande zote za Mkataba zinakubaliana kama ifuatavyo:

1.0 Mkataba huu unajumuisha na kuhusisha majadiliano yote yaliyofanyika kwa maandishi na pande zote mbili na utachukuliwa pamoja na Makubaliano yote yaliyoafikiwa kati ya pande zote mbili kabla na baada ya Mkataba huu.

1.1 Barua ya awali ya maombi ya kutoka kwa MPANGAJI kwenda kwa MPANGISHAJI.

1.2 Barua ya majibu kutoka kwa MPANGISHAJI kwenda kwa MPANGAJI.

1.3 Barua ya MPANGAJI kukubali (Acknowledge) kutekeleza matakwa ya MPANGISHAJI kabla ya kuingia kwenye makubaliano.

2.0 <u>**MUDA WA MKATABA**</u>

MPANGAJI amekubali kupanga eneo hilo kwa dhumuni la biashara kama ilivyoainishwa katika **kipengele C** hapo juu kwa kipindi cha miezi (12)........ kulingana na masharti na vigezo vilivyoainishwa hapo chini.

3.0 <u>**GHARAMA ZA ENEO**</u>

MPANGAJI atawajibika kulipa Kodi ya Shilingi za kitanzania 500,000/= Kwa mwezi ambayo ni sawa na Shilingi za Kitanzania 48,000,000/= kwa Miezi KUMI NA MBILI (12)

## 4.0 MALIPO

4.1 MPANGAJI atafanya malipo ya kila mwezi, Shilingi za Kitanzania ..500,000/=.. ikiwa ni gharama ya eneo kwa muda wa mwezi mmoja (01)

4.2 Namna ya Malipo

Malipo yote yanayohusiana na Mkataba huu yatafanyika kupitia Benki na atawasilisha stakabadhi ya malipo kwa MPANGISHAJI ifuatavyo:-

4.2.1 Jina la Mwenye Akaunti :- ..671 SAM REJIMENTI..........

4.2.3 Benki :- ..CRDB BANK..........

4.2.4 Akaunti Na :- ..0150626738000..........

## 5.0 SUB – LEASE CONTRACT

Kwamba MPANGAJI haruhusiwi kumpangisha au kubadilishana upangaji na mtu mwingine eneo hilo la biashara alilopangishwa bila kibali cha maandishi kutoka kwa MPANGISHAJI.

## 6.0 HUDUMA NYINGINEZO (UTILITIES SERVICES)

### 6.1 Maji na Umeme

Endapo MPANGAJI atahitaji huduma ya maji/Umeme atawasilisha ombi lake kwa MPANGISHAJI na Mita zote zitakazofungwa zitafungwa kwa jina la MPANGISHAJI.

6.2 Kwamba MPANGAJI atafanya malipo ya umeme na maji kupitia namba za mita atakazopatiwa na MPANGISHAJI kulingana na matumizi yake mwenyewe.

6.3 **Taka na Mazingira**

MPANGAJI atatakiwa kuliweka eneo pamoja na mazingira ya eneo la biashara katika hali ya usafi na usalama wakati wote ikiwemo na upandaji wa miti ya kivuli.

7.0 MPANGAJI hataruhusiwa kufanya shughuli zozote zisizo halali au biashara haramu katika eneo hilo, na endapo atahitaji kubadili aina ya biashara tofauti na biashara iliyoainishwa katika kipengele B atamtaarifu MPANGISHAJI na kuingia Mkataba upya.

8.0 **HAKI YA KUTUMIA ENEO**

8.1 MPANGAJI mara baada ya kutimiza masharti yote ya Mkataba huu ikiwa ni pamoja na kulipa ada zote kwa wakati. MPANGISHAJI hatambugudhi MPANGAJI katika kipindi chote cha malipo ya Mkataba huu.

8.2 MPANGISHAJI anahaki ya kufanya ukaguzi wa eneo hilo mara baada ya kutoa taarifa kwa MPANGAJI kuhusu utekelezaji huo kwa lengo la kufanya tathmini ya usalama na hali ya mazingira ya eneo hilo.

9.0 **UHAULISHAJI WA JENGO (TRANSFER OF BUILDING)**

9.1 MPANGAJI atamkabidhi Eneo la biashara MPANGISHAJI mara baada ya Mkataba wake kumalizika likiwa katika hali ya awali kama alivyokabidhiwa .

9.2 MPANGAJI atawajibika na ukarabati kwa uharibifu utakao sababishwa na yeye mwenyewe au jamii yake na endapo ukarabati

huo utaathiri sura na ramani ya awali ya eneo hilo basi MPANGAJI lazima apate kibali na maelekezo kimaandishi kutoka kwa MPANGISHAJI.

9.3 Endapo MPANGAJI atafanya ujenzi wowote ule utahesabika kama ujenzi wa muda (Temporary Building). MPANGAJI hatoruhusiwa kujenga makazi ya kuishi katika eneo hilo.

## 10.0 KUHUISHA MKATABA (RENEW OF CONTRACT)

Endapo MPANGAJI atahitaji kuendelea na Mkataba huu mara baada ya kipindi cha miezi ..12.......... kumalizikia atapaswa kutoa taarifa (NOTICE) ndani ya siku 15 kwa njia ya maandishi kabla ya Mkataba huu kumalizika.

## 11.0 KUVUNJWA KWA MKATABA HUU (TERMINATION OF CONTRACT)

11.1 Endapo MPANGAJI atahitaji kusitisha Mkataba huu atalazimika kutoa taarifa (NOTICE) kwa MPANGISHAJI kwa njia ya maandishi ndani ya siku 15 kabla ya kusitisha Mkataba akieleza sababu za kusitisha Mkataba.

11.2 Endapo taarifa ya maandishi imewasilishwa na upande mmoja upande wa pili utaifanyia kazi taarifa hiyo ndani ya siku kumi na nne (14) za kazi tangu kuwasilishwa kwake.

11.3 MPANGAJI ataondoka na kukabidhi eneo kulingana na Ibara 9.1 ya Mkataba huu inavyoelekeza.

11.4 MPANGAJI atahakikisha kuwa haachi madeni baki (**Outstanding Bills**) zake zozote endapo hatohitaji kuendelea na Mkataba

11.5 MPANGAJI hatodai fidia au gharama zozote alizotumia kuwekeza kwenye eneo hilo.

11.6 Endapo itatokea MPANGAJI amefariki dunia kabla ya kumalizika kwa Mkataba huu Msimamizi wa mirathi au Mrithi atapaswa kuheshimu Mkataba huu mpaka utakapo malizika. Msimamizi wa mirathi au Mrithi anahaki ya kuchagua kuendelea au kusitisha Mkataba huu.

## 12.0 **MATUKIO YASIYOTARAJIWA**

MPANGAJI atakuwa tayari kuachia Eneo hilo wakati wowote ule endapo MPANGISHAJI atahitaji Eneo hilo kwa matumizi mengine .

## 13.0 **USULUHISHI**

13.01 Endapo kutatokea kutoelewana/Mgogoro wowote kutokana na utekelezaji wa majukumu ya Mkataba huu, upande mmoja utatoa taarifa (notice) ya mgogoro huo kwa maandishi kwa upande mwingine ndani ya siku saba (07) ukitaka upande uliokiuka makubaliano haya kurekebisha kasoro hiyo ndani ya siku kumi na tano (15) toka tarehe ya kupokea taarifa ya kuwepo kwa mgogoro huo.

13.02 Endapo pande za mkataba huu zimeshindwa kutatua mgogoro huo kidiplomasia baina yao ndani ya siku kumi na tano (15), mgogoro huo utafikishwa ndani ya wapatanishi aliyeteuliwa na pande

zote mbili ambaye hafungamani na upande wowote ndani ya siku kumi na tano (15) toka siku ya kushindwa kutatua mkataba huo. Pande zote zitahakikisha zinafikia muafaka na kutatua mgogoro huo ndani ya siku kumi na tano (15) kwa njia ya makubaliano (Mediation).

13.03 Endapo pande zote mbili zitashindwa kufikia muafaka katika vikao vya upatanishi ndani ya siku kumi na tano (15) kwa Mpatanishi huru, basi Mgogoro husika utawasilishwa mbele ya **WASULUHISHI HURU**. Wasuluhishi hao watatatua mgogoro husika ndani ya siku kumi na tano (15) na uamuzi utakuwa na mwisho.

14.0 **MAREKEBISHO (AMENDMENT)**

Kwamba Mkataba huu utapitiwa kila baada ya MWEZI MMOJA (01) kwa ajili ya kupitia vipengele vya kodi, dharura au mahitaji na maendeleo mbali mbali ya Jeshi (MPANGISHAJI).

15.0 **SHERIA ITAKAYOTUMIKA**

Mkataba huu ni halali na utatafsiriwa kwa mujibu wa Sheria za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

16.0 Mwendelezo wa Mkataba huu utamaanisha kwamba malipo kamili yamefanyika.

17.0 MPANGAJI ataheshimu sheria zote na taratibu halali zinazokubalika na jamii/Nchi ili kudumisha usalama wa watu na mali zao. Jukumu la ulinzi na usalama wa mali zake ni jukumu la MPANGAJI mwenyewe.

**HIVYO BASI KWA USHAHIDI HUU**:- Mkataba huu unathibitisha kwamba, pande zote mbili zimekubaliana kwa hiari yao na kuweka saini zao hapo chini mbele ya Mashahidi kwa tarehe husika katika siku, mwezi na mwaka ifuatavyo:-

**671 REGT**

Jina: AYUBU SELEMANI RAMADHANI

(Mwakilishi aliyeidhinishwa)

Madaraka: MKUU WA REJIMENTI

Saini: ..........

Tarehe: 01/07/2025

KAMANDA REJIMENT 671 REGT 01 JUL 2025 S. L. P. 3142 DAR ES SALAAM

**SHAHIDI**

Jina: MASHAKA REXONA NYAGANZA

Madaraka: AFISA MRADI

Saini ..........

Tarehe: 01 JULAI 2025

**IMPERIAL ROAD HAULAGE LIMITED**

Jina: MUJTABA BHARWANI

(Mwakilishi aliyeidhinishwa)

Madaraka: DIRECTOR

Saini: ..........

Tarehe: 1/7/2025

IMPERIAL ROAD HAULAGE LTD P. O. Box 2150 DAR ES SALAAM TANZANIA

**SHAHIDI**

Jina: DAVID FARID RWEGASIRA

Madaraka: MWANASHERIA

Saini ..........

Tarehe: 1/7/2025

David Farid Rwegasira P.O.Box 8447 Dar es Salaam Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths